

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5  
Fax No. +255 026 2322624  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Kamati za Bunge zitakutana Jumatatu tarehe 19 Agosti hadi tarehe 02 Septemba 2019, Jijini Dodoma kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 3 Septemba 2019. Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai (Mb), ameziita Kamati hizo kuanza shughuli zake tarehe hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

**a) UCHAMBUZI WA MISWADA YA SHERIA**

Miswada Mitatu (3) ya Sheria inatarajiwa kujadiliwa na Kamati mbili (2) zilizopelekewa Miswada hiyo kwa mujibu wa **Kanuni ya 84(1)**. Kamati na Miswada hiyo ni kama ifuatavyo:-

- i) Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa itachambua na kujadili 'Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019' [**The e-Government Bill, 2019**];
- ii) Kamati ya Katiba na Sheria itachambua na kujadili miswada **miwili** ambayo ni 'Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa Mwaka 2019' [**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2019**]; na 'Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2019' [**The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2019**];

**b) KUPOKEA TAARIFA MBALIMBALI ZA WIZARA/TAASISI**

Kamati tisa (9) za sekta na Kamati ya Bajeti zitachambua Taarifa za Taasisi/ Wizara za Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa mujibu wa Kifungu cha **7(1)**, **kifungu** cha **7(2) (i) (ii) (iii)** na **(iv) na Kifungu** cha **9(a)** vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

### **c) UCHAMBUZI WA TAARIFA YA CAG**

Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma ambazo ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018.

### **d) UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO**

Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo itachambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkuutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Madhumuni ni kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika **Kifungu cha 11** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

### **e) UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itachambua Taarifa ya Uwekezaji wa taasisi/mashirika Saba (7) kwa mujibu wa **Kifungu cha 12 (a) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge pamoja na Miswada itakayoshughulikiwa na Kamati katika kipindi hiki vinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz).

Imetolewa na:                   Kitengo cha Mawasiliano na Uhuriano wa Kimataifa  
   Ofisi ya Bunge  
**DODOMA**

16 Agosti, 2019.